




Likizo kwa bibi!



Violet Otieno

Catherine Groenewald

Brigid Simiyu

swahili

nivå 4

(uten bilder)



Barnebøker for Norge

[barnebok.no](http://barnebok.no)

Likizo kwa bibi!

Skrevet av: Violet Otieno

Illustrert av: Catherine Groenewald

Oversatt av: Brigid Simiyu

Denne fortellingen kommer fra African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) og er videreformidlet av Barnebøker for Norge ([barnebok.no](http://barnebok.no)), som tilbyr barnebøker på mange språk som snakkes i Norge.

Dette verket er lisensiert under en Creative Commons

[Navngivelse 4.0 Internasjonal Lisens.](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/deed.no)

<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/deed.no>




Odongo na Apiyo waliishi mjini na baba yao.  
Walisubiri likizo kwa hamu. Siyo tu kwa shule  
kufungwa, bali ni kwa sababu walienda  
kumtembelea bibi yao. Aliishi katika kijiji cha uvuvi  
karibu na ziwa kubwa.



Odongo na Apiyo walichangamka kwani ulikuwa wakati wa kumtembelea bibi kwa mara nyingine. Usiku huo, walipanga mizigo yao na kujiandaa kwa safari ndefu ya kwenda kijijini. Hawakuweza kulala ila waliongea usiku kucha juu ya likizo yao.




Mapema asubuhi iliyofuata, waliondoka katika gari la baba yao kuelekea kijijini. Walipita milima, wanyama pori na mashamba ya majani ya chai. Walihesabu magari na kuimba nyimbo.




Odongo na Apiyo waliporudi shuleni, waliwasimulia marafiki zao kuhusu maisha ya kijijini. Baadhi ya watoto waliamini kuwa maisha ya mjini ni mazuri. Wengine waliamini kijijini ni bora zaidi. Lakini zaidi ya yote, kila mmoja alikubali kwamba Odongo na Apiyo walikuwa na bibi wa kipekee.

Odongo na Apiyo walimkumbatia kwa pamoja na kumaga.




Baada ya muda, watoto walichoka na kusinzia.






Baba aliwaamsha Odongo na Apiyo walipofika kijijini. Walimkuta bibi yao, Nyar-Kanyada, akipumzika kwenye mkeka chini ya mti. Kwa Dholuo, Nyar-Kanyada maana yake ni 'binti wa watu wa Kanyada'. Alikuwa ni mwanamke mrembo na imara.



Baba yao alipokuja kuwachukua, hawakutaka kuondoka. Walimuomba Nyar-Kanyada aende nao mjini. Alitabasamu na kusema, "Nimezeeka, siyawezi ya mjini. Nitasubiri mje kijijini kwangu tena."




Nyar-kanyada aliwakaribisha ndani kwa kucheza na kumba kwa furaha. Wajukuu wake walikuwa na shauku ya kumpa zawadi walizomitea kutoka mjini. "Fungua yangu kwanza," Odongo alisema. "Hapana, yangu kwanza!" Apiyo akasema.



Likizo ilikaribia kuisha na watoto walitakiwa kurudi mjini. Nyar-kanyada alimpa Odongo kofia na Apiyo sweta. Aliwafungia chakula cha kula safarini.



Baada ya kufungua zawadi, Nyar-Kanyada aliwabariki wajukuu wake kitamaduni.




Mwisho wa siku walikunywa chai pamoja. Walimsaidia bibi yao kuhesabu pesa alizozipata.






Kisha Odongo na Apiyo wakaenda nje.  
Waliwakimbiza vipopeo na ndege.




Siku nyingine watoto walikwenda sokoni pamoja  
na Nyar-Kanyada. Nyar-Kanyada alikuwa na  
kibanda cha kuuza mboga, sukari na sabuni. Apiyo  
alipenda kuwatajia wateja bei za bidhaa. Odongo  
aliwafungia wateja bidhaa walizounua.




Walipanda kwenye miti na kurushiana maji ziwani.



Asubuhi moja, Odongo aliwapeleka ng'ombe wa bibi yake malishoni. Wakakimbilia ndani ya shamba la jirani. Mwenye shamba alikasirishwa sana na Odongo. Akatishia kuwazuia ng'ombe kula mimea yake. Tangu siku hiyo, Odongo alihakikisha kwamba ng'ombe hawaingii matatani tena.




Nyar-kanyada aliwatundisha wajukuu wake jinsi ya kupika ugali mwepesi wa kula na mchuzi. Aliwaonesha namna ya kupika wali wa nazi wa kuliwa na samaki wa kukaanga.



Giza Iilipoingia, walirudi nyumbani kwa ajili ya chakula cha jioni. Kabla hata ya kumaliza kula, walikuwa wanasinzia!



Siku iliyofuata, baba yao alirudi mjini na kuwaacha na Nyar-Kanyada.



Odongo na Apiyo walimsaidia bibi yao na kazi za nyumbani. Walichota maji na kuokota kuni. Walikusanya mayai ya kuku na kuchuma mboga za majani kutoka kwenye bustani.